HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI

# HAI YETU

JARIDA TOLEO L A JULAI—SEPTEMBA 2022









# ZAIDI YA BILIONI TATU KUMALIZA TATIZO LA MAJI HAI



*Rais wa jamhuri ya muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan akiongea na wakazi wa kata ya Bo mang'ombe wilayani Hai.*

Wananchi wa kata ya Muungano wilayani Hai mkoani Kilimanjaro wanamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan baada ya kuanza kupata maji katika eneo hilo kufuatia kukabiliwa na adha ya muda mrefu ya upatikanaji wa huduma ya maji .

Akizungumza katika mahojiano maalumu Mwananchi wa kata ya Muungano Amon Ngowi ameeleza kuwa ana furaha ambayo hawezi kuielezea baada ya kuanza kupata maji kwa saa 24 bila ya mgao kwani mara ya mwisho kupata maji katika bomba lililopo nyumbani kwake ilikuwa mwezi Mei 2021.

"Namshukuru sana Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan na mbunge wetu Saashisha Mafuwe lakini pia namshukuru diwani wangu ambaye ni mwenyekiti wa Halmashauri ya Hai Edmund Rutaraka ambapo kwa kweli kwa juhudi zao tumeona, nilifunga bomba mwaka jana mwezi wa 5 na tangu nimefunga bomba halijawahi kutoa maji, kuanzia sasa ninapata maji bila mgao, ni furaha kwangu na kwa familia pamoja na majirani kwani eneo letu hili lilikuwa sugu".

Naye mkazi wa Kibaoni kata ya Bomang'ombe Said Nasibu anasema kuwa kwa sasa anapata maji kwa wingi tofauti .



*Mradi wa maji wa Kikafu -Soka katika utekelezaji.*

na hapo awali ambapo maji yalikuwa ya mgao na wakati mwingine walikuwa hawapati maji kabisa katika eneo hilo huku akielekeza pongezi zake kwa viongozi.

"Namshukuru sana mbunge wetu Saashisha Mafuwe kwa kufikisha kilio chetu cha muda mrefu kwa Mhe. Rais Samia na sasa tunapata maji namshukuru pia mwenyekiti wa halmashauri Edmund Rutaraka pamoja na diwani wetu wa kata ya Bomang'ombe Evod Njau wameupiga mwingi sana kwenye suala la maji"

Mbunge wa jimbo jimbo

la Hai Saashisha Mafuwe kwa nyakati tofauti akiwa Bungeni jijini Dodoma- amekuwa akiuliza Maswali kutaka kujua ni lini Serikali itajenga mradi mkubwa wa maji utakaomaliza kero ya maji kwenye kata tatu za Bomang'ombe Muungano na Bondeni.

Baada ya sakata hilo la maji la muda mrefu - kutua mezani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, hatimaye akapita katika mji wa Bomangombe na kusalimiana na wananchi katika eneo la stendi ya Sanya na kuwaeleza wakazi hao kuwa ;

"Najua sijamaliza tatizo la maji ndani ya Bomang'ombe, lakini kuna mradi mkubwa tunaupanga pamoja na halmashauri ya Hai, mradi wa biloni 3 kuhakikisha kwamba tunaleta maji maeneo yaliyobaki ndani ya Bomang'ombe".

Wilaya ya Hai ,Mkoani Kilimanjaro kwa muda imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji katika kata za Bomang'ombe, Muungano na Bondeni, ambapo kufuatia kukamilika kwa mradi mkubwa wa maji katika chanzo (chem chem) ya kikafu–soka uliogharimu kiasi cha zaidi ya shilingi Bilioni tatu (3,392,463,389) unatarajiwa kumaliza tatizo hilo la maji katika kata hizo.

# ZAIDI YA BILIONI 1.9 ZATUMIKA KUJENGA NA KUKARABATI MIUDOMBINU YA AFYA HAI



***Naibu waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel, akiwa anazungumza na viongozi mbalimbali wa wilaya ya Hai kwenye ziara yake ya kikazi ,katika kikao kidogo ofisini kwa mkuu wa wilaya ya Hai.***

Halmashauri ya wilaya ya Hai imepokea jumla ya fedha shilingi bilioni 1.9 za miradi ya maendeleo Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kutoka serikali kuu, pamoja na mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Afya.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa miradi ya Afya mbele ya Naibu waziri wa Afya - Dkt. Godwin Mollel, Mkuu wa wilaya ya Hai Mhe. Juma Irando amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzani Mhe. Samia Suluhu Hassan Kwa kuiwezesha wilaya hiyo katika ujenzi wa miundombinu ya huduma za kijamii na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

Irando ameeleza kuwa kwa ngazi ya wilaya zipo hospitali mbili ambazo ni hospitali ya wilaya na Hospitali ya Machame -



*Mkuu wa wilaya ya Hai Mhe. Juma Said Irando akiwa anazungumza kwenye kikao cha ziara ya Naibu waziri wa Afya Dkt Godwin Mollel wilayani Siha.*

inayomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), vituo 8 vya afya kati ya hivyo 7 vinamilikiwa na Serikali na kituo kimoja 1 cha mtu binafsi, Zahanati 57 huku 23 zinamilikiwa na mashirika, 29 zinamilikiwa na Serikali , na 5 zinamilikiwa na watu binafsi.

“Katika mwaka wa fedha 2020/21 kwenye masuala ya kinga, tiba na miundombinu, Halmashauri kupitia Sekta ya Afya imewapatia wananchi 144,128 chanjo ya UVIKO 19 kati ya lengo na wananchi 158,673 sawa na 90.8%” amesema Irando.

Kwa upande wake Naibu waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel ameitaka divisheni ya Afya na viongozi wa wilaya hiyo -kushirikiana ili kutimiza lengo la kutoa huduma stahiki za Afya kwa wananchi kwa kuzingatia kanuni, sheria na maadili.

“Napenda kuwapongeza Mkuu wa Wilaya (Juma Irando) na mbunge wa jimbo la Hai (Saashisha Mafuwe) kwa kuonesha ushirikiano kwenye Idara ya Afya pamoja na mapokezi mazuri, pia mjitahidi katika masuala ya bima ya afya, mkifanya kitu kizuri muache taarifa hapa hata mtu akija kulalamika kuwepo na taarifa kama ushahidi”

Naibu waziri Wa Afya Dkt. Godwin Mollel katika ziara yake wilayani Hai ametembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa kituo cha afya unaoendelea katika kata ya Masama kati ambapo-

hadi sasa umepokea kiasi cha fedha shilingi milioni 20 kati ya milioni 50 za makusanyo ya ndani ya halmashauri zilizotengwa. Ujenzi wa kituo hicho cha afya hadi kukamilika kwake kitagharimu zaidi ya shilingi milioni 700.



*Naibu waziri Dkt.Godwin Mollel akizungumza na Mmoja wa Madaktari wakati wa Ziara yake wilayani siha.*



*Mmoja wa washiriki akiwa anachangia hoja kwenye ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo.*

# PIKIPIKI 34 ZA MKOPO ZAKABIDHIWA KWA VIJANA



*Pichani aliyekatikati mwenye kofia ya bluu ni mbunge wa Jimbo Hai Mhe Saasisha Mafuwe akikabidhi mkopo wa vifaa(pikipiki) kwa vijana ,wanawake na watu wenye ulemavu , Hai.*

Mbunge wa jimbo la Hai Saashisha Mafuwe amemshukuru Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa miradi mingi aliyoipeleka katika kila sekta ndani ya wilaya ya Hai.

Mbunge Saashisha ametoa shukrani hizo wakati akikabidhi mkopo wa pikipiki wenye thamani ya shilingi milioni 119 kwa vikundi vya vijana wanawake na watu wenye ulemavu ambapo mkopo huo unatokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri hiyo.

Ametoa rai kwa vijana waliopata mikopo ya pikipiki kuzitumia katika malengo yaliyokusudiwa na kuwataka kuwa mfano katika kuzingatia sheria za usalama barabarani.

Mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya ya Hai Edmund Rutaraka amempongeza mkurugenzi wa halmashauri hiyo pamoja na baraza la madiwani kwa usimamizi madhubuti wa mapato yanayopatikana ambapo pamoja na mambo mengine husaidia upatikanaji wa mikopo hiyo.

Aidha, Mwenyekiti wa CCM wilaya ya Hai Wang'uba Maganda ameeleza kuwa chama hicho kina Sera ya uchumi mzuri ulioimarika kwa ajili ya watu wake, ikiwa ni pamoja na wanawake vijana watu wenye ulemavu huku akiwataka wanufaika wa mikopo hiyo kuitumia kwa weledi ili kujiimarisha kiuchumi.

Mikopo hiyo ya pikipiki 34 ilitolewa ikiwa ni agizo la kisheria linalozitaka halmashauri zote nchini kutenga asilimia 10 ya mapato yake ya ndani na kutoa mikopo hiyo kwa wananchi kwa lengo la kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo na kujinufaisha kiuchumi.



***Mbunge wa wilaya ya Hai Saashisha Mafuwe (aliyevaa miwani nyeusi) akiwa miongoni mwa msafara wa pikipiki zikifanyiwa majaribio.***

# RUZUKU PEMBEJEO ZA KILIMO KULETA SHANGWE KWA WAKULIMA WILAYA YA HAI



*Afisa kilimo wilaya ya Hai David Lekei akiwa anazungumza kwenye mahojiano maalumu kuhusiana na ruzuku ya pembejeo za kilimo .*

Zaidi ya wakulima 30,000 wanatarajiwa kunufaika na ruzuku ya pembejeo inayotolewa na Serikali katika msimu wa kilimo mwaka 2022/2023.

Akizungumza katika mahojiano maalumu mkuu wa divisheni ya kilimo, mifugo na uvuvi wilaya ya Hai, David Lekei amesema ili wakulima waweze kupata ruzuku hiyo wanapaswa kujisajili kwenye mfumo wa kidigitali ambao utawezesha kutambua wakulima wote wilayani humo ambao wanaweza kupata pembejeo za kilimo kwa bei ya punguzo la Serikali.

"Niwaombeni wakulima wilayani hapa hakikisheni mnajiandikisha kwenye ofisi za watendaji wa vijiji na kata, orodha itakayotoka kwenye ofisi hizo ndio itakayotumika kupata huduma za pembejeo za ruzuku "Alisema Lekei.

"watakaoshindwa kujisajili na majina yao kukosekana kwenye orodha watakosa huduma ya ruzuku ya pembejeo"Alisisitiza Lekei

Alisema kuwa Serikali iliamua kutumia mfumo wa kidigitali katika mpango wa ruzuku ya mbolea - ili kuongeza ufanisi kwa wakulima na kuwaondolea mzigo kutokana na upandaji wa pembejeo hizo.

Hadi kufikia mwezi septemba mwaka huu 2022 jumla ya wakulima 22,900 wilayani Hai walikuwameshasajiliwa kwenye mfumo huo, wakulima wote walipaswa kujisajili katika kipindi hicho ili kutumia vema fursa hiyo ya pembejeo za kilimo kwa bei ya punguzo la Serikali.

# MBUNGE HAI KUTIMIZA NDOTO YA HAI YA VIWANDA



(*Kulia*) ***ni mbunge wa jimbo la Hai Mhe Saashisha Mafuwe akiwa na mwekezaji wa kiwanda cha uchakataji wa maparachichi .***

Zaidi ya wakazi 3000 wa wilaya ya Hai wanatarajiwa kunufaika na ajira kupitia mpango wa ujenzi wa kiwanda cha kisasa cha uchakatajia wa zao la Parachichi kinachotarajiwa kujengwa wilayani Hapo.

Hayo yameelezwa na mbunge wa jimbo hilo Saashisha Mafuwe katika mahojiano maalum akiwa wilaya ya Hai.
Mhe Saashisha alieleza kuwa toka alipoomba ridhaa ya kuliongoza jimbo la Hai ndoto yake ilikuwa kuifanya wilaya ya hiyo kuwa ya kilimo na viwanda hivyo anafanya kazi kwa nguvu zake zote kuhakikisha ndoto hiyo inatimia.

“Jambo ambalo ni uhitaji kwetu sisi ni Hai ya kilimo na viwanda ilituweze kupata kiwanda tumeshirikiana na wenzetu wa TASAF na waziri wa kilimo na mifugo Hussein Bashe tumepata mdau alieonesha nia ya kujenga kiwanda hapa kwetu Hai na kitakuwa kiwanda kikubwa cha kipekee Africa mashariki cha kuchakata zao la parachichi na bidhaa mbali mbali zinazotakana na zao hilo”

Alisema kuwa hatua iliyopo kwa sasa ni mchakato wa kufuata matakwa ya kisheria kwa mkutano mkuu wa bodi ya ushirika kukaa kwa kufuata taratibu za vyama vya ushirika ili waweze kutolea maamuzi na baraka.

“Mwekezaji huyu yuko tayari muda wowote kuanza ujenzi wa kiwanda hicho lakini pia nimshukuru sana Mheshmiiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo sasa wizara ya kilimo imebadilika sasa haionekani kilimo ni adhabu kwa sasa kilimo ni tija na watu wanahamasika kulima na kuwekaza katika kilimo”

Aidha mbunge huyo pia alieleza kuwa ameshatembelea masoko makubwa na uuzaji wa bidhaa za kilimo katika nchi tofauti tofauti Afrika na nje ya bara hili na kujiridhisha kuwa mazao ya wakazi wa Hai yanaweza kuuzwa katika maeneo hayo.

# TAASISI YA AL ATA'A YAZINDUA KAMBI YA MATIBABU YA SIKU 3, MGENI RASMI DC, HAI.




*Mkuu wa wilaya ya Hai Mhe Juma Said Irando akiwa anazungumza na wananchi wakati wa uzinduzi wa zoezi la upimaji wa Afya bila malipo kwa wananchi katika hospitali ya wilaya ya Hai .*

Mkuu wa wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro Mhe. Juma Irando aliishukuru taasisi ya misaada ya Al Ata'a inayofadhiliwa na shirika la Qatar Charity kwa kuweka kambi ya matibabu katika hospitali ya wilaya ya Hai kwa lengo la kutoa huduma za matibabu kwa wananchi.

DC Irando aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa kampeni ya utoaji msaada wa matibabu kwa wananchi kwa kuwezeshwa na taasisi hiyo ambayo iliweka kambi ya matibabu siku 3 bila malipo katika hospitali ya wilaya hiyo.

Mkuu huyo wa wilaya alitoa rai kwa wadau wengine wa Afya walioko ndani na nje ya mkoa wa Kilimanjaro kuona umuhimu wa - Kutoa huduma ya afya kwa wananchi kwani maendeleo ya taifa huletwa na jamii yenye Afya njema huku akiwataka wananchi kujitokeza kupatiwa huduma hizo.

Mkurugenzi mtendaji wa taasisi ya misaada ya Al Ata'a Ahmed El hamrawi alieleza nia yake ya kuendelea kuunga mkono jitihada za kutoa misaada ya matibabu na kuahidi kurejea tena kwa ajili ya kuweka kambi ya matibabu ya macho.

Aidha Mganga mkuu wa wilaya ya Hai Dkt. Itikija Msuya alieleza kuwa siku ya kwanza katika zoezi hilo walijitokeza zaidi ya watu 136 kupatiwa huduma ambapo -



*Mganga mkuu wa hospitali ya wilaya ya Hai Dkt. Itikija Msuya akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa zoezi la upimaji wa Afya bila malipo kwa wananchi .*

wamegundua kuwa watu wengi wanasumbuliwa zaidi na magonjwa ya kisukari, presha, moyo na shinikizo la damu.

Kwa upande wake Mganga mfawidhi wa hospitali ya Wilaya hiyo Dkt Grace Ntogwisangu akitoa taarifa ya huduma za Afya kwenya hospitali hiyo aliishukuru taasisi ya misaada ya Al Ata'a kwa kuwezesha kutoa huduma za matibabu bila malipo kwa - wananchi.

Taasisi ya misaada ya Al Ata'a inayofadhiliwa na shirika la Qatar Charity iliweka kambi ya matibabu katika hospitali ya wilaya ya Hai kuanzia Julai 14 hadi 16, 2022 kwa lengo la kutoa msaada wa matibabu bila malipo katika magonjwa yasiyoambukiza huku wakilenga kuwafikia watu 500.




***Mwenyekiti wa BAKWATA wilaya ya Hai Omari Mahmudu akiwa anazungumza wakati wa uzinduzi zoezi la upimaji wa Afya bila malipo kwa wananchi katika hospitali ya wilaya ya Hai***

# DED HAI ATAKA WATUMISHI WAPYA KUFUATA TARATIBU ZA KAZI



*Pichani ni waajiriwa wapya kutoka kada mbalimbali waliohudhuria semina elekezi kuhusiana na utumishi wa umma*

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai Dionis Myinga amewataka watumishi wapya walioajiriwa katika kada mbalimbali kwenye halmashauri hiyo kufuata sheria, taratibu, miongozo pamoja na maelekezo yanayotolewa na viongozi wa ngazi za juu katika majukumu yao ya utumishi.

Myinga aliyasema hayo katika ukumbi wa halmashauri ya Wilaya ya Hai wakati akiwapokea waajiriwa wapya 76 wa kada mbalimbali waliofika katika semina elekezi kuhusiana na utumishi wa umma.

Aidha mkurugenzi huyo aliwataka watumishi hao kufanya kazi kwa weledi, uzalendo na nidhamu ili kuonesha matokeo halisi kwa wale waliowapatia ajira hizo.

Kwa upande wake aliyekuwa mkuu wa idara ya utumishi wa umma Maria Kivelia aliwataka watumishi hao kuzingatia maadili ya utumishi wa umma ikiwemo kuvaa mavazi yanayostahili kuvaliwa wawapo kazini sambamba na kuonesha ushirikiano kwa wale watakaowakuta katika vituo vyao vipya vya kazi.

Kwa upande wao watumishi wapya wameishukuru serikali kwa kuaminika na kuajiriwa kuzitumikia nafasi hizo na wameahidi kufanya kazi kwa uweledi, na kufuata sheria na taratibu za utumishi wa Umma.

Semina hiyo iliyofanyika kwa lengo la kutoa mafunzo kwa watumishi hao wapya walioajiriwa kwa mwaka 2022 imejumuisha kada mbalimbali ikiwemo watumishi wa afya 35, utawala 11 pamoja na kada ya elimu watumishi 30.

# WANANCHI WATAKIWA KUSHIRIKI KWENYE MIRADI YA MAENDELEO

Kamati ya ulinzi na usalama wilayani Hai Mkoani Kilimanjaro iliwataka wananchi kushiriki kwenye miradi ya maendeleo inayoendelea ili kujua thamani yake kwani miradi hiyo inatekelezwa Kwa ajili Yao.

Akizungumza wakati wa ziara ya kamati hiyo Mkuu wa wilaya ya Hai Juma Said Irando aliwataka viongozi wanaosimamia miradi ya maendeleo kwenye ngazi ya Vijiji, Vitongoji, kata na wilaya kuhakikisha wananchi wanashirikishwa na kujua thamani ya miradi hiyo.

“Niwashukuru wazazi Kwa hatua ya kushirikiana na serikali Kwa ajili ya manufaa ya watoto wanaosoma hapa na watakaokuja kujiunga kusoma katika madarasa haya, viongozi hakikisheni mnawashirikisha hawa wananchi kwasababu miradi inayoletwa na Mhe. Rais ni kwa ajili ya wananchi, nawapongeza sana endeleeni na ushirikiano huo huo”Mhe. Irando

Aidha Irando aliwataka waliopewa kazi ya kuisimamia miradi hiyo kuhakikisha wanaisimamia na kuikamilisha kwa wakati kwani



*Mkuu wa Wilaya ya Hai Mhe. Juma Said Irando akiwa anazungumza na wananchi na viongozi mbalimbali wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo.*

mradi unapochukua mda mrefu huleta hasara kutokana na kubadilika kwa gharama na vifaa vya ujenzi kila mara.

Kwa upande wake Katibu tawala wa wilaya ya Hai Upendo Wella alisema ni utaratibu wa kamati ya ulinzi na usalama kutembelea miradi hiyo lengo ni kuona yanayoendelea na si kuishia kupokea taarifa huku akiwataka wananchi kuiunga mkono serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kushiriki kazi zinazoendelea katika miradi hiyo.

“Imekuwa kawaida yetu sisi Kama kamati ya ulinzi na usalama kutembelea na kukagua miradi ya mandeleo katika wilaya yetu lakini katika maeneo tuliyopita kukagua ujenzi unaendelea kwa hatua nzuri, rai yangu kwa wananchi kushiriki kuiunga mkono serikali kwa kazi ambazo zinafanywa kwani serikali haiwezi kufanya kazi peke yake” Upendo Wella

Baadhi ya miradi iliyotembelewa na kamati hiyo ni pamoja na Ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu sita ya vyoo shule ya msingi Kikavu chini ambao -

upo kwenye hatua ya umaliziaji,ujenzi wa nyumba za walimu(two in one),ujenzi wa darasa moja ambalo linatokana na nguvu za wananchi ambapo pia serikali iliunga mkono umaliziaji wa ujenzi huo.



***Mhandisi Arnod Matandiko mwenye reflekta akiwa anamuelezea mkuu wa wilaya namna hatua za mradi zinavyoenda.***



***Ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa , shule ya msingi Kikavu chini ambao ni miongoni mwa mradi wa maendeleo.***



***Ujenzi wa vyoo vya shule ya msingi kikavu chini ambao ni miongoni mwa mradi wa maendeleo.***

# MASALIA ZAIDI YA 2000 YA BINADAMU KUREJESHWA

Umoja wa Machifu hapa nchini unakusudia kuyarejesha masalia ya binadamu ikiwemo mafuvu ya Vichwa zaidi ya 32 yaliyopo Ujerumani yaliyochukuliwa wakati wa utawala wa wajerumani lengo likiwa ni kuyaenzi na kuongeza pato la taifa kupitia utalii.

Katika tamasha la utamaduni lililofanyika Januari mwaka huu, 2022 Machifu hao walimuomba Rais Samia Suluhu Hassan ambaye Pia ni Chifu mkuu wa Machifu Tanzania, kurejeshwa masalia hayo ambapo Rais aliziielekeza wizara zinazohusika kuchukua hatua stahiki ili kurejesha masalia hayo.

Katibu wa Machifu mkoa wa Kilimanjaro Joseph Msele akizungumza kwenye maonyesho ya marejesho hayo yaliyofanyika Septemba 10, 2022 Kyalia Machame wilayani Hai, alisema kwamba "Tumepata taarifa nzuri kutoka kwa watanzania wanaoishi Ujerumani ambao nao wamekuwa na harakati kama hizi, ambapo katika juhudi hizo chini ya kikundi cha Berlin Post Colonial, tayari wamepata idhini ya awali kwamba hivyo vitu vinaweza kurudishwa"

"Kwa taarifa ni kwamba Berlin pekee kuna mafuvu ya binadamu zaidi ya 22 na kwa mji mwingine ulioko mpakani mwa Ufaransa kuna mafuvu zaidi ya 32



*Pichani ni Joseph Mselle katibu wa machifu mkoa wa kilimnjaro,Mnyaka Mboro , Said Omary, Grabriel Orio na Judica Munisi wakiwa kwenye maonesho– chunguzi ya histioria ya ukoloni Kilimanjaro na Meru*

na haya ni yale ambayo yanahusu ukanda wa kaskazini kwa maana yana lebo ya Chaga, lakini vitu vingine ambavyo ni vya jadi vipo zaidi ya 300 na kwa Tanzania nzima ni zaidi ya 2000"

Diwani wa kata ya Machame Kaskazini Judica Mushi akizungumza katika maonesho hayo alieleza kuwa hakuna haja mafuvu hayo kuendelea kukaa Ujerumani, ni wakati sasa wa kuyarudisha ili watanzania waweze kuyaenzi kwa lengo la kuleta kumbukumbu nzuri na kitega uchumi katika masuala ya utalii.

Akiwasilisha salam za mkuu wa wilaya ya Hai Juma Irando, Afisa tarafa ya Machame Said Izina amewapongeza viongozi walioandaa maonesho hayo ya kuenzi utamaduni kwani husaidia huonyesha ni wapi watanzania wametoka na kipi wanapaswa kupambania kiujumla.

# AFISA MAENDELEO YA JAMII ATOA MBINU ZA KUKABILI UKATILI NA UNYANYASAJI KWA WATOTO



***Mmoja kati ya watoto ambao wamefanyiwa ukatili.***

Wazazi na walezi wameaswa kuwa karibu na watoto wao kipindi cha likizo na nyakati nyingine katika kuhakikisha wanakua na maadili mazuri katika kupunguza matukio ya unyanyasaji na ukatili kwa watoto.

Hayo yamebainishwa na Afisa maendeleo ya Jamii kata ya Masama Rundugai wilaya ya Hai Saumu Daffa ,ambapo amesema hapo awali wawakilishi kutoka ustawi wa jamii pamoja na polisi walikuwa wakitoa elimu endelevu kuhusiana na ukatili wa jinsia kwa watoto.

Aidha amesema wazazi wengi wameshindwa kufanya jukumu la malezi kwa kutokuwa karibu na watoto na - kuwaachia walimu jukumu hilo, huku wengi - wao wakikimbizana na jukumu la kutafuta pesa jambo ambalo linawapa wakati mgumu walimu kuwa karibu na watoto kama wazazi.

Ameongeza kuwa maeneo ya kata ya Masama Rundugai kumekuwa na wimbi kubwa la watoto kutoka jamii ya wafugaji, wengi wao wakiwa sokoni wakiuza bidhaa mbalimbali wakati wa likizo na kwenda kwenye vijiwe vya kuonesha Tv jambo linanohatarisha usalama wao

Hata hivyo amesema elimu inayotolewa imeleta mafanikio makubwa kutokana na kupungua kwa idadi ya watoto wanaoenda sokoni muda wa masomo na huku wengine wakiendelea kupewa elimu zaidi ili kuhakikisha watoto wanapata haki zao za msingi.

# WANANCHI WASISITIZWA KUHIFADHI CHAKULA HAI




***Katibu tawala wilaya ya Hai Upendo Wella akiwa anazungumza kwenye wiki ya maadhimisho ya elimu ya watu wazima.***

Suala la Elimu ni jukumu la kila mmoja hivyo hata watu wazima wanastahili kuelimika zama hizi, kila mwaka huwa kuna maadhimisho siku ya elimu ya watu wazima.

Katibu tawala wilaya ya Hai Upendo Wella ametoa msisitizo huo Kwa wananchi wilayani humo alipohutubia katika kilele cha maadhimisho ya wiki ya Elimu ya watu wazima yaliyofanyika Mkoani Kilimanjaro katika kata ya Weruweru.

Aidha katibu tawala Upendo Wella ameyatumia maadhimisho hayo kuwataka wananchi kuhifadhi chakula kutokana na hali ya ukame unaoendelea na kupelekea wakulima wengi kupata mavuno kidogo na wengine kukosa mazao kabisa katika msimu uliopita wa kilimo.

“Msisitizo kwa Serikali ni kwamba kile Kidogo ambacho umepata ni vyema kutunza kwani kuna wengine ambao hawakupata kabisa, na hali ya chakula kwa msimu unavyoendelea inawezekana isiwe nzuri, tunajua bei ya mahindi sasahivi imekuwa juu sana na kwa mkulima hiyo ndiyo tija ila kuuza huku tukijua tunatakiwa kuhifadhi chakula”

Kwa upande wake mkuu wa divisheni ya Elimu ya awali na msingi wilaya ya Hai Hussein Kitingi akizungumza kwenye kilele cha maadhimisho hayo amewakumbusha wazazi -

na walezi kuwa Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watu wazima MEMKWA ni wa bure na watoto wanaokusudiwa ni wale wenye umri wa miaka 10 hadi 13.

Naye Afisa Elimu ya Watu wazima wilaya hiyo Emmaculata Mgaza ameeleza kuwa wameweka mkakati wa mpango wa kutoa mafunzo ya aina mbalimbali Kwa watu wazima hususani katika masuala ya kilimo, mifugo na malezi.

Maadhimisho ya wiki ya Elimu ya watu wazima yameongozwa na kauli mbiu isemayo "**Kujifunza kusoma, Kuandika na Kuhesabu, Yatakayozingatia Ubora na Ujumuishi wa Makundi yote"**.




*Katibu Tawala wilaya ya Hai Upendo Wella akiwa anakagua kazi mbalimbali zinazotekelezwa na vikundi katika maonesho ya wiki ya elimu ya watu wazima.*

# MKUU WA WILAYA AWATAKA WAALIMU KUZINGATIA MAADILI YA KAZI



*Mkuu wa wilaya ya Hai Mhe. Juma Saidi Irando akiwa anazindua vitabu mkakati vya kuboresha elimu.*

Mkuu wa wilaya ya Hai Mhe. Juma Irando alizindua vitabu vya Mkakati wa kuboresha Elimu nchini katika Halmashauri ya wilaya ya Hai huku akiwataka Walimu kuzingatia maadili ya kazi zao.

Uzinduzi huo ulifanyika Septemba 16, 2022 wakati wa kikao Cha wadau wa Elimu wilayani Hai kilichofanyika kwenye Ukumbi wa chuo cha Ufundi Kilimanjaro Modern wilayani humo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo uliokwenda sambasamba na kugawa vitabukwa Maafisa Elimu kata, Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu, DC Irando ameeleza kuwa vitabu hivyo vitatumika kama mwongozo katika utendaji wao wa kazi.

“Niseme vitu vichache kwa ajili ya muongozo kwa mfano mwalimu kushindwa kumaliza mada, kumkatisha tamaa mwanafunzi, kuchanganya lugha, hilo naomba wadhibiti ubora mkalisimamie, tusimamie misingi ya lugha, lakini pia niwasisistize usiri na uaminifu katika utekelezaji wa majukumu yenu”

Katibu Tawala wilaya hiyo Upendo Wella alitoa rai Kwa waalimu hao kuhakikisha wanaitumia miongozo hiyo ambayo imezinduliwa katika ngazi ya wilaya ili kutimiza lengo lililokusudiwa.



*Katibu Tawala wilaya ya Hai Upendo Wella akiwa anazungumza wakati wa uzinduzi wa vitabu mkakati vya kuboresha elimu.*

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya Hai David Lekei amewataka walimu kufanyakazi kwa kuzingatia miongozo ili kuendelea kudumisha rekodi nzuri ya Elimu ndani ya wilaya hiyo.

Naye mkuu wa Divisheni ya Elimu Sekondari Julius Mduma alieleza kuwa vitabu hivyo vitakuwa na kigezo cha kupima mwenendo wa ufundishaji kwa Shule za msingi na Sekondari.

“Vitu hivi ambayo vimeandaliwa hapa vinaonesha vigezo vitakavyotumika wakati wa uteuzi wa waalimu katika nyadhifa mbalimbali”



*Wazazi, walezi na walimu wakiwa kwenye uzinduzi wa vitabu mkakati wa kuboresha elimu.*

# KATIBU MKUU APOKEA SHUKRANI ZA WANANCHI BAADA YA UJENZI WA KITUO CHA AFYA CHA CHEKIMAJI



*Nyumba ya watumishi ambayo ni nyumba moja yenye uwezo wa kuchukua familia tatu .*

Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo alisema kazi ya serikali ni kutafuta namna ya kushughulikia na kutatua kero zinazokabili jamii kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo na wananchi.

Chongolo alitoa kauli hiyo wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi aliyoifanya katika Kata ya Masama Rundugai wilayani Hai, na kukagua kituo cha afya cha Chekimaji kinachojengwa kwa fedha kutoka serikali kuu, wananchi pamoja na mchango wa Halmashauri .

Kauli hiyo imekuja baada ya wananchi wa kata hiyo kuishukuru serikali kwa ujenzi wa kituo cha Afya cha Chekimaji ambacho walisema kitaondoa adha ya wananchi kwenda umbali mrefu kwa ajili ya kutafuta huduma ya matibabu.

Chongolo pia aliwataka wananchi kuhifadhi chakula Kwa ajili ya matumizi ya familia ili kuzuia tatizo linaloweza kujitokeza la kukosa chakula Kwa baadhi ya jamii na kuwataka kutotumia mazao ya chakula kutengenezea pombe za kienyeji.

Alisema mwaka huu kumekuwa na changamoto ya ukame jambo ambalo limeathiri mavuno na kuwataka wananchi kuhakikisha wanatunza chakula walichokipata, amewataka pia wafugaji kuuza baadhi ya mifugo yao kipindi hiki ambacho bado ina hali nzuri ili fedha watakazo pata wanunue chakula na kukihifadhi ndani kwa matumzi ya baadae.

Awali akisoma taarifa ya ujenzi wa kituo hicho mkuu wa divisheni ya huduma za Afya ,Ustawi wa Jamii na Lishe wa Wilaya ya Hai Dkt. Itikiji Msuya alisema ujenzi wake ulianza 2010 na utakamilika mwaka huu huku kikitarajiwa kuhudumia wananchi 14,000.

# MADIWANI WAMETAKIWA KUSIMAMIA MIRADI YA MAENDELEO

Madiwani Halmashauri ya Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro wametakiwa kuisimamia miradi ya maendeleo iliyopo kwenye kata zao na kuhakikisha inamalizika kwa wakati na kwa ubora.

Hayo yalisemwa na mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Hai Edmund Rutaraka kwenye baraza la madiwani lililofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo.

Rutaraka alisema halmashauri hiyo imefanikiwa kukusanya asilimia 94 ya mapato kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ikiwa ni ongezeko la asilimia 12 kwa mwaka wa fedha uliopita ambapo waliweza kukusanya asilimia 82.

Akizungumza katika kikao hicho, Mbunge wa Jimbo la Hai Saashisha Mafuwe amewapongeza madiwani kwa utendaji wao wa kazi ikiwa ni pamoja na usimamizi wa miradi ya maendeleo.

Aidha mbunge huyo amemtaka Meneja wa Tanesco wilaya ya Hai kuhakikisha wanashirikiana kikamilifu na viongozi wa mradi wa maji Bomang'ombe – Kikafu soka ili kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati.

# KATIBU TAWALA APONGEZA KAMATI YA CHANJO, HAI

Katibu tawala wilaya ya Hai Upendo Wella aliipongeza kamati ya Afya ya msingi ya wilaya hiyo kwa namna walivyotekeleza kwa ufanisi majukumu waliyopewa ya kuhakikisha zoezi la chanjo linafikiwa kulingana na malengo yaliyopo.

Aliyasema hayo wakati akizungumza kwenye kikao chenye lengo la kuonyesha namna kampeni ya chanjo ya polio ilivyofanikiwa sambamba na Mwenendo wa chanjo ya uviko 19 kwenye ukumbi wa halmashauri ya wilaya ya Hai.

Naye Mratibu wa chanjo wilaya ya Hai Alice Mchelo ameeleza kuwa kampeni ya chanjo ya polio kuzuia ugonjwa wa kupooza kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano wilayani humo imefanikiwa kwa asilimia kubwa ukilinganisha na malengo waliyopewa.

"Lengo lilikuwa ni kuchanja Watoto 35,992 ambao ni watoto wote waliokuwa chini ya umri wa miaka mitano katika wilaya yetu ya Hai, lakini tumefanikiwa kuwafikia Watoto 38,928 ambayo ni sawa na asilimia 108.16 ya lengo tulilopewa" amesema mratibu huyo wa chanjo.

Wilaya ya Hai ni moja ya wilaya zilizotekeleza kampeni ya chanjo ya matone ya polio ili kuzuia ugonjwa wa kupooza kwa awamu ya pili iliyofanyika kuanzia Mei 18 -21, 2022.

# MKUU WA WILAYA YA HAI KUHIMIZA ZOEZI LA SENSA



*Mkuu wa wilaya ya Hai Mhe. Juma Saidi Irando akiwa kwenye zoezi la Sensa ya watu na makazi.*

Katika kuhamasisha zoezi la sensa ya watu na makazi lililofanyika agosti 23 mwaka huu viongozi wilayani Hai walitumia nafasi zao kuwasisitiza wananchi juu ya umuhimu wa kushiriki kikamilifu katika zoezi hilo.

Mkuu wa wilaya ya Hai Juma Irando ambaye ndiyo Mwenyekiti wa kamati ya Sensa ya wilaya hiyo alipokuwa akihamasisha wananchi wilayani humo kushiriki zoezi la Sensa akasema ,

" Niwaombe wananchi wa wilaya ya Hai tutoe taarifa sahihi kwa Makarani na timu nzima ya Sensa katika wilaya yetu muda utakapofika, kuhesabiwa ni muhimu kwa maendeleo yetu hivyo tujiandae kuhesabiwa"

Mbunge wa Hai Saashisha Mafuwe yeye alifanikiwa kuzungumza na makundi mbalimbali ikiwemo waendesha bajaji na bodaboda ambapo aliwaambia kwamba

" Waendesha bajaji na bodaboda mtusaidie kupeleka ujumbe kwa abiria wote wilaya ya Hai kwamba tarehe 23 Agosti 2022 ni siku ya kuhesabiwa, tutulie nyumbani tuhesabiwe au pale ulipo"

Saashisha akaongeza kuwa "Kuanzia Sasa ukibeba abiria wakati anashuka mwambie kumbuka kuhesabiwa tarehe 23 kuhesabiwa ni dili, kuhesabiwa ni maendeleo.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya hiyo Edmund Rutaraka -

katika mahojiano maalumu aliwahamasisha wananchi kuhesabiwa akisema "hakuna nchi yoyote inayoweza kupanga mipango ya maendeleo bila kuwa na Takwimu sahihi za watu wake"

Katibu Tawala wilaya hiyo Upendo Wella katika kuhamasisha zoezi la Sensa akasema kwamba "Sensa ni zoezi muhimu katika kuisaidia Serikali kupeleka maendeleo kwa wananchi kulingana na idadi kamili ya watu wa eneo husika hivyo kila mmoja ajiandae kuhesabiwa bila kuacha hata mtu mmoja"

Aidha baadhi ya Makarani wa Sensa wanaeleza kuwa baada ya viongozi hao kuhamasisha wananchi kwa wingi kupitia mikutano mbalimbali pamoja na kituo cha Redio Boma Fm, imesaidia sana wananchi kupata uelewa na kupelekea zoezi hilo kufanyika kwa urahisi

Sensa ya watu na makazi ni zoezi ambalo hufanyika hapa nchini kila baada ya miaka 10 ambapo mnamo Agosti 23, 2022 zoezi hilo lilifanyika nchini kote na katika wilaya ya Hai Sensa ilifikia asilimia 90. 86.

Aidha sababu kuu ya zoezi hilo kufikia zaidi ya asilimia 90 katika wilaya ya Hai ni hamasa kutoka kwa viongozi mbalimbali wa wilaya hiyo wakieleza juu ya umuhimu wa wananchi kuhesabiwa.



***Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Hai Edmund Rutaraka akiwa anahesabiwa kwenye zoezi la sensa ya watu na makazi.***

# MATUKIO KWA PICHA

## BARAZA LA MADIWANI LIKIWA KWENYE KIKAO CHA ROBO YA MWAKA






# MATUKIO KWA PICHA

## UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO





JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI.

S.L.P 27, Hai ,Kilimanjaro, Tanzania

www.haidc.go.tz

Hai Dc

http://radiotadio.co.tz/bomahaifm

Radio Boma Hai Fm 89.3 Mhz